Mungu Akijitambulisha Mwenyewe Kwa Tabia Zake

Kwa namna fulani nilishangaa kumwona rafiki yangu, Joseph Boze, pale, ndipo nikageuka na kuchukua muda mfupi kumpa mkono.

2 Hebu tugeuke sasa katika Neno la Mungu, kwenye Waebrania, mlango wa 1. Ninataka kusoma, kwa sehemu, kifungu cha 1, cha 2, na cha 3, ili kutoa somo kwa ajili ya usiku.

> *Mungu, ambaye alisema* zamani *za kale na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia mbalimbali,*
>
> *Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwanawe, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*
>
> *Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vitu vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha*. . .*aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;*

3 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Na sasa katika Uwepo Wake wa Kiungu, kama una haja yoyote ambayo ungetaka ijulikane Kwake, naomba uinue tu mkono wako, na hilo ndilo ombi lako, kwamba Mungu ataninii . . .

4 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa mbele ya kiti Chako cha enzi, kwa imani katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Nasi tumepewa hakikisho hili, kwamba, "Tukiomba lolote katika Jina Lake, litatimizwa." Nawe unajua shauku zetu na haja zetu, Nawe umeahidi ya kwamba utatupatia yote tunayohitaji. Kwa hiyo, Baba, tungeomba kama ulivyotufundisha, "Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yatendeke duniani, kama ilivyo Mbinguni." Kwamba ombi letu, usiku wa leo, liweze kuwa ni kulingana na mapenzi Yako kutupa, na utujalie fadhila hizi. Lipake mafuta Neno, Bwana, na wanenaji wote na wasikilizaji, na jalia Roho Mtakatifu aingie na awe mwenye kulitekeleza Neno, usiku wa leo, miongoni mwetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Ketini.

5 Kesho asubuhi, naelewa, ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel. Kwa kawaida, mahali walipo na tawi, nina majaliwa ya kuzungumza kwenye kiamshakinywa chao. Hadi wakati huu, hilo ndilo shirika la pekee, ambalo

si dhehebu, bali, kundi la pekee ambalo mimi—mimi ni mwanachama wake, ni Wafanya Biashara Wakristo. Na sasa mimi huwazungumzia tu, kimataifa.

6 Sasa, usiku wa leo, tunatumaini ya kwamba kukusanyika huku hakutakuwa ni bure. Nimewajia, mchovu, koo lililochoka, na kupata homa kidogo kutokana na . . .

7 Nimetoka Tucson ambako kweli ni kuzuri na kukavu, kisha nikaja hapa na kweli ni kuzuri na kunanyesha, kwa hiyo kuna tofauti kubwa. Kama ninyi nyote mnayo maji yote huku, kama mngeyapeleka kwetu, tungeshukuru. Bali hamwezi kufanya hilo, hakika.

8 Lakini ninawaambia jambo moja, kuna fumbo hapo. Vitu vye—vye—vyetu vyote huko Arizona, miti yetu, imejaa miiba. Kila kitu kina mwiba. Ni kwa sababu ni kukavu. Sasa kama kichaka hicho hicho kingalikulia hapa, lingekuwa ni jani zuri la kupendeza. Mnaona, halina maji, hiyo ndiyo sababu linakuwa mwiba.

9 Na wakati Kanisa linapokosa Maji ya Uzima, linakuwa kavu na linachoma, pia, linachoma na kupiga kila kitu. Lakini ambapo Maji ya Uzima yanatiririka, hulifungua jani hilo na kulifanya jororo, laini na tamu, takatifu na linalompendeza Mungu. Kwa hiyo hebu Bwana Mungu na atumwagilie maji, usiku wa leo, tusije tukawa miiba; bali tutakuwa majani mazuri ambayo watu wakaidi wangeweza kuketi chini ya mti wa kivuli chetu na kupata pumziko kwa nafsi zao.

10 Sasa nataka kuchukua somo, usiku wa leo, Bwana akipenda, nami ninaivuta maskini maikrofoni hii karibu niwezavyo, kwa sababu ya ukosefu wa sauti. Ninataka, kutokana na kusomwa huku kwa Waebrania 1:1, ninataka kuchukua somo la: *Mungu Akijitambulisha Mwenyewe Kwa Tabia Zake*. Hebu nirudie hilo tena, kwa kuwa ninajua sauti haisikiki vizuri hapa. Mungu hujitambulisha Mwenyewe kwa tabia Zake.

11 Sasa, karibu kila kitu hutambulikana kwa tabia zake. Nami nina Maandiko machache hapa ambayo ningeninii . . . na muhtasari, ambao ningetaka kuurejea. Sasa, tabia ya kitu chochote hutambulisha kile kilicho.

12 Sasa, kama katika maumbile yote, maua hutambulishwa, mara nyingi, kwa tabia zake. Kama yakiwa karibu, spishi moja kwa nyingine, tabia ya ua hilo itatambulisha ni ua la aina gani. Na katika wanyama mwitu, mara nyingi . . .

13 Mimi, mimi ni mwindaji. Nawe huna budi kujua tabia ya mnyama unayemwinda, ama wakati mwingine hakika unaweza kudanganyika. Kwa mfano, kama Kondoo Jiwe huko juu kabisa British Kolumbia. Nilikuwa tu chini ya Yukon majira haya yaliyopita ya kupukutika majani, baadhi ya ndugu waliopo hapa sasa walikuwa pamoja nami, nasi tulikuwa tukiwinda.

14 Sasa kama hukujua tofauti, wakati ulipokuwa ukimfuata kondoo ama kulungu, usingeweza kujua tofauti yake isipokuwa ulikuwa mwindaji mwerevu sana. Kwa sababu, wanafanya miburuzo inayofanana; wanarukaruka wanapokimbia. Kisha unamwona mmoja amesimama kwenye umbali fulani, huku amekificha kichwa chake, mbona, i—ingekuwa vigumu kujua tofauti. Tako lao lina karibu upana sawa; ni jeupe, kama tu la kulungu. Ingekuwa ni vigumu sana kuwatofautisha. Ila pembe zake huitambulisha tabia yake, kwa pembe hizo. Kondoo ana pembe iliyo mviringo, naye kulungu ana pembe zilizochongoka. Na jambo lingine, kulungu asingepanda juu hivi, kula.

15 Na halafu mbuzi, akitembea, pia, kuna tabia katika mbuzi, na kondoo, ambayo ingekubidi ujue tofauti yao, wakati ukiwa huko juu, kwa kuwa wote wanaishi juu mlimani. Inakubidi kujua tofauti. Bali ukiangalia, mbu—mbuzi hujikwaa anapotembea; ambapo, kondoo huweka miguu yake chini *hivi*, anapotembea. Sifa bainifu ya jinsi anavyofanya mburuzo wake. Unamtambua mnyama wako kwa tabia za yale anayofanya, na jinsi atendavyo, na kile anachokula, na kadhalika. Hujitambulisha kwa tabia yake. Halafu ukimruka mmoja, na kuangalia kile anachofanya, unaweza kujua jinsi wanavyoenda. Unaweza kujua kwa tabia ya mnyama mwingine.

16 Basi ulipata kuona, sijui kama mnao hapa au la, ndege manjano; vema, gogota ndilo jina zuri kwao, na ndege jay. Ndege jay ana karibu ukubwa wa ndege manjano. Na ukiwaona hao wawili wakiruka, hao ni kama ndege wa aina moja. Kama usingeweza kuiona rangi, bali uwaangalie tu, unaweza kujua ndege manjano ni yupi. Ndege jay huruka, takriban, kwa njia ya mkato. Lakini ndege manjano, hupigapiga mabawa yake; anapopiga mabawa yake, yeye hushuka kisha anapanda, kushuka kisha kupanda. Mnaona, yeye huruka-ruka, namna *hiyo*, nawe unaweza kujua hiyo ndiyo tabia ya ndege manjano, jinsi anavyoruka.

17 Ukiangalia kwa—kware anapotokea, jinsi anavyojitokeza. Halafu angalia kama uko katika kinamasi, ambamo huenda kuna kware, na ninii—na kichenge. Ninyi wawindaji mnajua hilo. Kichenge wa Wilson na kichenge wa jaki, wanajitambulisha kwa jinsi wanavyotokea na jinsi wanavyoenda. Wanajitambulisha kwa tabia yao ya kuruka, kwamba hao ni ndege wa aina gani. Kwa hiyo, kama ukiwasikia tu, unaweza kujua tu alikuwa ni yupi, jinsi alivyojitokeza, kwamba ni yupi, kwa tabia yake ya kuruka.

18 Kama vile mwanamume na mwanamke. Wote ni wanadamu, bali mwanamke ana tabia tofauti na mwanamume. Nilikuwa nikisoma hapa, wakati fulani uliopita, kuhusu Sulemani na yule malkia. Sijapata kufikia kuuhubiri maskini Ujumbe wangu hapa, kwenu, juu ya malkia wa Kusini, akipanda kuja kumwona Sulemani, na kuona hiyo karama ya utambuzi. Nilikuwa

nikisoma kuhusu hicho, hapa si muda mrefu uliopita, nao wakasema, kwamba, “Moja ya mafumbo yaliyowekwa mbele ya Sulemani, lilikuwa, malkia huyu alimchukua mwanamke, ama wanawake, hasa, na kuwavisha kama mwanamume.”

19 Sasa, hilo lilikuwa ni la kigeni siku hiyo, bali hakika ni la kisasa, leo hii. Na—nanyi mnajua hilo ni kosa. Biblia ilisema ya kwamba mwanamke hapaswi kufanya hivyo. “Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume.” Naye Mungu asiyebadilika alisema hivyo, kwa hiyo hiyo ni kweli.

20 Kwa hiyo tunaona ya kwamba Sulemani, mara alipowaangalia, aliwafanya watembee ama wafanye jambo fulani, na papo hapo akasema, “Ni wanawake.” Mnaona, angeweza kujua kwa tabia ya mwanamke huyo, jinsi alivyojiendesha, kwamba alikuwa ni mwanamke wala si mwanamume.

21 Na halafu karibu kila kitu ndivyo kilivyo, kwa tabia zake. Kama tu vile watu wengi ni wenye kutumia mkono wa kushoto, na wenye kutumia mkono wa kulia. Wana sifa ya vile wanavyojiendesha. Unaweza kujua kama ni mtu mwenye kutumia mkono wa kulia ama wa kushoto, kwa jinsi wanavyojiendesha, jinsi wanavyovifikia vitu kwa mkono huo wa kushoto ama wa kulia.

Pia kumbukeni, Yesu alikuwa na kitu kama hicho, ambacho . . .

22 Mikono miwili iko karibu . . . Inafanana. Ina alama za vidole gumba sawa, alama za vidole, vidole vitano; kidole kidogo, cha shahada, na kadhalika. Kama tu vile mkono wa kulia na mkono wa kushoto ilivyo na vidole vya namna ile ile, kwa kawaida, ukubwa ule ule wa mkono, kabisa. Na tofauti pekee iliyopo, kwayo, ni kwamba mmoja ni wa kushoto na mwingine wa kulia. Hiyo ndiyo tofauti pekee unayoweza kuona. Mmoja ni wa kushoto, mwingine ni wa kulia.

23 Kwa hiyo basi katika jambo hilo, Yesu alisema . . . Huenda nikaingiza jambo moja dogo hapa. Yesu alisema, katika Mathayo 24, kwamba, “Tabia za Roho huyo zingekuwa kwa namna fulani zinafanana katika siku za mwisho, zitakaribiana sana hata zingewadanganya walio wateule kama yamkini.” Mnaona, wangeninii tu . . .

24 Hebu chukua mkono wako uuinue tu juu. Unaona, usipotambua, mmoja unafanana na mwingine, kwa kila njia, ila mmoja ni wa kushoto na mwingine wa kulia.

25 Hivyo ndivyo roho zilivyo katika siku ya mwisho. Kwa namna fulani zinafanana, bali zina tabia inayozitambulisha. Moja ni ya kweli, na nyingine ni ya uongo, nayo inaweza kutambulishwa kwa tabia yake.

26 Roho wa Mungu anaweza kutambulishwa kwa tabia Yake. Mnaona? Roho wa Mungu, na roho wa kanisa. Kunaye roho wa kanisa, na Roho wa Mungu ambaye hafanani na roho wa kanisa, hata kidogo.

Kuna roho wa kimadhehebu.

27 Kuna roho ya kitaifa. Kuna roho ya taifa. Kila taifa, ninapoenda mle, ukitembea mle, unapata roho nyingine. Nilienda Finland, watu wazuri, bali kulikuwako na roho ya Kifini. Nikashuka nikaingia Ujerumani, kuna roho ya Kijerumani.

28 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikienda pamoja na mke wangu, wakati tulikuwa tungali tunaishi Indiana, miaka kadhaa iliyopita, tukaenda kwenye maskini duka kuu. Nilikuwa tu nimerudi nyumbani. Ilitubidi kwenda kununua chakula. Basi nilipokuwa njiani kwenda kule, tulininii . . . Ulikuwa ni msimu wa kiangazi, huenda usiamini hili, bali tulimwona mama aliyekuwa amevaa gauni. Na hilo lilikuwa ni jambo la kigeni sana, mimi . . . Lilinishtua sana. Ni—nikasema, "Angalia pale, hiyo yaonekana ya kigeni, mwanamke yule amevaa gauni." Hao wengine walikuwa wamevaa mavazi ambayo hayakuninii . . . hayakumpasa mwanamke. Ndi—ndipo akasema . . . Nikasema, "Vema, hiyo ni roho tu ya Kimarekani, mnaona, roho ya Marekani."

29 Sasa, roho ya Marekani, ni ninii . . . linadhaniwa kuwa ni taifa la Kikristo, bali roho ya taifa hili si ya Kikristo. Huenda likaitwa taifa la Kikristo, bali ni maili milioni moja kutoka kwake, katika tabia. Kwa hiyo, mwanamke huyu, nikasema . . .

Akasema, "Vema, hivi sisi si Wamarekani?"

30 Kasema, nikasema, "La. Tunaishi hapa. Hii ni nchi yetu. Tu—tu—tunakaa humo. Tunaipenda. Ndilo taifa lililo bora kuliko yote ulimwenguni. Lakini, hata hivyo, sisi si Wamarekani." Nikasema, "Tumezaliwa kutoka Juu. Roho Mtakatifu alishuka chini, nasi ni wa Ufalme fulani. Si wa ulimwengu huu." Nikasema, "Hiyo ndiyo sababu dada zetu wanavaa magauni, wana nywele ndefu, hawajipodoi. Unaona, tabia zao zinawatambulisha kama 'utakatifu kwa Bwana,' kutoka Juu."

31 Hivyo basi, tunautafuta Ufalme. Tunamtafuta Mfalme aje na kuwapokea raia Wake kwenye Ufalme Wake. Nao wanatambulikana kwa tabia za—zao, kwamba hazina zao si za ulimwengu huu ama za taifa hili. Zinatoka juu, Utukufuni. Kwa hiyo, wao, "Wanautazamia Mji ambao Mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu." Wametambulishwa vizuri.

32 Laiti ningalikuwa na sauti ya kutosha kuwahubiria usiku fulani. Lakini ni—ninaliondokea hilo. Sasa, kutambulishwa kwa tabia zake.

33 Tunapata mfano mzuri hapa katika wakati wa Israeli, walipoingia kwenye nchi ya ahadi. Naye Mungu alikuwa amewaita sawasawa na ahadi Yake. Akamwambia Ibrahimu ya kwamba, angeninii . . . uzao wake ungekuwa kwenye taifa hili la kigeni, kwa miaka mia nne, na kisha angemkomboa kwa mkono mkuu wenye nguvu. Nao wangeenda kwenye nchi fulani, basi, waliyoahidiwa, iliyojaa maziwa na asali. Ndipo basi wakati wa ile ahadi ulipokaribia, akaja Fa—Farao asiyeitambua huduma kuu ya Yusufu aliyokuwa nayo miongoni mwao.

34 Na, hili, Mungu akamwinua nabii jina lake Musa. Naye mtu huyu alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri. Hapana shaka bali alikuwa mtu mkuu, mwerevu, mwenye akili, kwa kuwa angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Alionekana ni mtu afaaye—aliyefaa sana kwa ukombozi.

35 Bali, mnaona, tunachokiita ukombozi, na kile Mungu anachokiita ukombozi, kuna tofauti.

36 Sasa mwangalieni mtu huyu na maadili yake yote. Alijua alizaliwa apate kuwakomboa wana wa Israeli. Hata hivyo, pamoja na elimu yake yote, hiyo ndiyo tu aliyojua kuhusu jambo hilo, na akijua kwamba alikuwa ameitwa na Mungu akafanye kazi hiyo, alikuwa na ninii yake yote . . . Alikuwa na Digrii yake ya Sanaa, na Ph.D. yake, na LL.D. zake, na kadhalika. Basi akatoka kwenda kuwakomboa Israeli, naye akashindwa kabisa.

37 Sasa angalieni, ilionekana kana kwamba, yeye akiwa na mguu wake kwenye kiti cha enzi huko Misri, kuwa Farao, kwamba angewakomboa wana wa Israeli baada ya kuwa Farao, kwa sababu alikuwa halifa kwenye—kwenye kiti cha enzi. Lakini, mnaona, kwamba, akifanya hivyo, lisingeitambulisha tabia ya Mungu katika ukombozi wa watu Wake.

38 Yeye alisema atawakomboa. *Yeye* "atawakomboa kwa mkono wenye nguvu," sio Musa kwa jeshi kuu, bali Mungu kwa Mkono wenye nguvu.

39 Tunaona ya kwamba nabii huyu alitoroka na alikuwa nyikani kwa muda wa miaka arobaini. Ilimchukua Farao miaka arobaini kuishindilia elimu ndani yake, na ikamchukua Mungu miaka arobaini kuibinya imtoke. Kwa hiyo tunaona, siku moja, kwamba yeye, huko nyuma ya jangwa, alikutana na Bwana Mungu katika kichaka kilichowaka moto, katika mfano wa Nguzo ya Moto katika kichaka. Ndipo akaagizwa kutoa viatu vyake, kwamba, mahali alipokuwa amesimama palikuwa patakatifu. Sasa mwangalieni mtu huyu mzuri, mstaarabu, mwenye elimu, aliyekuwa, angalieni mabadiliko ya tabia zake baada ya kukutana na Mungu. Alifanya lililo ninii sana . . .

40 Wakati mwingine Mungu hufanya mambo kwa njia rahisi sana, na kwa njia ya kijinga sana, kwa mawazo ya kimwili. Angalieni mtu aliyekuwa ameshindwa kabisa; huku amezungukwa na majeshi yote ya Misri na kila kitu apate

kufanya mapenzi ya Mungu, pamoja na elimu yake yote, kwenye umri wa miaka arobaini, katika umri wake ulio bora. Huyu hapa, umri wa miaka themanini, kesho yake asubuhi, pamoja na mke wake ametagaa juu ya nyumbu, akiwa na mtoto kwenye paja lake, na fimbo mkononi mwake, akishuka kwenda Misri, kuiteka. Nena kuhusu tamasha la dhihaka! Lakini hiyo ilikuwa ikionyesha tabia za Mungu, kwa kuwa alikuwa na mtu ambaye angeliamini Neno Lake. Hivyo tu. Jambo ni kwamba, ungeweza kuwazia uvamizi wa mtu mmoja ukielekea Misri, ambako, jeshi lilikuwa limeshindwa? Lakini ilikuwa ni kitu gani? Tabia yake, mbinu zake zilibadilika. Alikuwa akienda katika Jina la Bwana, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO." Jambo ni kwamba, aliiteka. Aliiteka, kwa kuwa alikuwa akienda katika Nguvu za Bwana.

41 Njiani mwake, akiwaongoza Israeli kutoka waende kwenye nchi ya ahadi, alikutana na ndugu yake, ndugu yake wa kimadhehebu, Moabu. Sasa, Moabu, hata kidogo, hawakuwa makafiri. Hao walikuwa ni watoto wa binti ya Lutu. Mmoja wa watoto wao ali—alizaa Moabu.

42 Sasa, huko juu, ninawataka myaone mataifa haya mawili, yakilinganishwa. Hii hapa Misri, kidogo, imetawanyika, hamna taifa la kuliendea, hamna watu mashuhuri wala mfalme, wala chochote kile, wala waheshimiwa miongoni mwao, ni watu tu wakielekea kwenye nchi ya ahadi. Na hapa iliwabidi kupitia kwenye nchi ya Moabu. Ilikuwa moja kwa moja kwenye mkondo wa ahadi.

43 Nao Moabu, pia, walikuwa waaminio wa Yehova, nao walikuwa na nabii. Nao Israeli walikuwa na nabii. Wote wawili walikuwa na manabii.

44 Na sasa angalieni, walikuwa wamefikia mahali ambapo nabii wa taifa lenye utaratibu alikuwa akishuka kuja kulilaani taifa hili lingine, kwa kuwa walikuwa wazururaji tu, wasio na Mahali maalum pa kuishi. Kwa hiyo walishuka wakaja.

Basi waangalie hao manabii wawili: Inapofikia kunena kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi kabisa. Kwa sababu, angalieni, Balaamu, yule askofu, aliwaambia, "Sasa nijengeeni madhabahu saba."

45 Saba ni nambari kamilifu ya Mungu, inayowakilisha Nyakati Saba za Kanisa, siku saba za uumbaji, kadhalika. Sasa angalieni, saba, Mungu anakamilika katika saba.

46 "Madhabahu saba, na juu ya kila madhabahu uweke fa—fahali mdogo." Sasa haya ni madhabahu yale yale waliyokuwa nayo huko chini kwenye kambi ya Israeli. Hao pale huko chini Israeli, wakiwa na madhabahu yale yale waliyo nayo hapa juu; na dhabihu ile ile, fahali kwa fahali; nabii kwa nabii. Mataifa mawili, yakilinganishwa.

47 Mfano mkamilifu kabisa wa siku tunayoishi, kama tungalikuwa na wakati wa kuliendea! Mwangalie Mungu

akifanya hili kwa fumbo, ambalo tutaliona, tukiyaweka sambamba.

48 Sasa, pia, Balaamu alihitaji kondoo dume juu ya kila madhabahu. Hiyo ilikuwa ikinena juu ya imani yake katika Masihi ajaye. Kondoo dume, kondoo wa kiume, hiyo ndiyo dhabihu ile ile waliyokuwa nayo huko Israeli; kule chini kwenye kambi ya Israeli, hapa juu kwenye—katika Moabu. Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi, bali, angalieni, kimsingi katika mafundisho.

49 Lakini nabii mmoja huko kwenye kambi ya Israeli alikuwa na tabia za Mungu na, Neno la Mungu. Alidumu na ahadi ya Mungu kwa ajili ya wakati huo, kwa kuwa alikuwa akielekea kwenye nchi ya ahadi. Mnaona?

50 Sasa, kwa upande wa kimsingi, Balaamu, Balaki angeweza kuwa ametambulishwa tu kama Musa alivyokuwa.

51 Lakini, unaona, Musa, akiwa ndiye nabii wa kweli wa Mungu, si kwamba tu alikuwa na sehemu za kimsingi, bali alikuwa na utambulisho wa Mungu. Mnaona, alikuwa kwenye jukumu lake, yale hasa yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo; si kwa wakati wa Nuhu, bali kwa wakati huo. "Nitawapeleka kwenye nchi iliyojaa maziwa na asali." Walikuwa njiani mwao, nao Israeli walitambulishwa pamoja na nabii wao, Musa, pamoja na Ujumbe wa wakati huo. Tabia za Mungu zilitambulishwa katika Musa. Nguzo ya Moto ilikuwa ikimfuata. Pia alikuwa na upatanisho ukitenda kazi; sio kunena habari zake; bali ulikuwa ukitenda kazi. Si yale yatakayokuwako; bali yaliyopo sasa hivi!

52 Angalieni, yeye alikuwa na nyoka ya shaba iliyokuwa imeinuliwa kwa ajili ya maradhi na magonjwa ya watu hao, kwa hiyo Musa alikuwa akitumia uponyaji wa Kiungu. Alikuwa na upatanisho, nyoka ya shaba ikiashiria kwamba Mungu alikuwa humo kambini, nao watu walikuwa wakiiangalia hiyo nyoka ya shaba na kuponywa.

53 Pia alikuwa na Mwamba uliopigwa ukimfuata. Na huo ulikuwa ukimtambulisha Mungu, kuyaweka Maji ya Uzima miongoni mwao, furaha na wokovu, kwamba wasingeangamia bali walikuwa na Uzima wa milele. Ilikuwa ni mfano wa . . . Ule Mwamba uliopigwa nyikani ulikuwa ni mfano wa Kristo akipigwa.

54 Halafu, walikuwa wakisafiri kulingana na ahadi. Huo ulikuwa ni utambulisho mwingine, wa kuonyesha tabia ya Mungu. Haidhuru hii nyingine ilikuwa ni ya kimsingi jinsi gani kwa Neno; yeye alikuwa na cha kimsingi, pamoja na utambulisho, na tabia ya Mungu miongoni mwao. Mungu alijitambulisha Mwenyewe. Manabii wawili, wote wawili ni manabii, na wote wawili ni wa kimsingi; bali Mungu alizitambulisha tabia Zake katika Musa, kwa kuwa alikuwa na tabia za Mungu pamoja naye.

55 Sasa, tena, tabia za Mungu sikuzote ni za kimbinguni, kwa kuwa Yeye ni wa kimbinguni. Mungu ni wa kimbinguni. Ni jambo lisilo la kawaida, daima, kwa mwelekeo wa mawazo ya siku hizi. Mnajua hilo. Mungu daima amevuruga mipangilio, kwa—kwa ajili ya makundi ya kidini katika kila wakati uliowahi kupita.

56 Na hakuna wakati mmoja mtu mmoja aliwahi au kundi la watu liliwahi kujiundia dhehebu juu ya ujumbe ambalo halikufa na kuwekwa kwenye rafu wala kamwe halikuinuka tena. Hamna historia. Walutheri, Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, na kadhalika, kamwe hawakuinuka tena, walipoanza kulifanyia makundi.

Mungu hujishughulisha na watu binafsi.

57 Angalieni, Yeye ni asiye wa kawaida sana kwa mwelekeo wa kimawazo. Mnaona, tunapotelea kwenye mtindo, nasi hatuna budi kuliamini *hivi*. Ndipo Mungu anakuja huko pamoja na Neno Lake aliloahidi, na kujitambulisha Mwenyewe kwenye Neno hilo. Kundi *hili* haliwezi kuliendea, kwa kuwa haliliamini. Mnaona, tayari limejitenga Nalo.

58 Kama vile Yusufu, yeye alikuwa ni mwana wa Daudi, na ni mtu mwema, Yusufu mume wa Mariamu. Alikuwa ni mtu mwema, na hapana shaka aliisoma Biblia, yale magombo, sikuzote, kwa kuwa. . .naye alikuwa akimtazamia Masihi kuja, na ilimpasa kujua yale Maandiko yalisema yangetukia. Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba."

59 Vema, sasa, yeye alikuwa akiambatana na msichana huyu mdogo, Mariamu, labda mwenye umri wa miaka kumi na minane, naye huenda alikuwa na umri mkubwa zaidi kidogo. Na ndipo walipoposana wapate kufunga ndoa, alionekana ni mja mzito. Sasa, kwa namna fulani hilo lilikuwa ni jambo gumu kwa Yusufu kutulia kuhusu hilo. Hapana shaka kwamba Mariamu alimwambia kuhusu kutembelewa na Gabrieli. Lakini tunaona, jinsi tabia yake ilivyokuwa ikimwongoza, alilitilia shaka.

60 Sasa alipatikana kuwa mja mzito kabla hawajafunga ndoa. Na, katika Biblia, adhabu hiyo ni kifo, kwa kupigwa mawe. Mwanamke asiyefunga ndoa kupata mimba, ilimpasa kupigwa mawe. Hakukuwapo umalaya Israeli. Uliondolewa. Kwa hiyo tunaona, katika Kumbukumbu la Torati, inatwambia hivyo.

61 Sasa tunaona ya kwamba, Mariamu, ilionekana kana kwamba alikuwa akijaribu kumtumia Yusufu kama tu kinga kwa tendo alilokuwa ametenda. Kwa sababu, kama alipatikana tayari ni mja mzito kabla hawajafunga ndoa, basi hana budi kupigwa mawe, naye hana budi kumpata mtu fulani sasa atakayesimama kama kinga kwa ajili yake. Na hilo lilionekana, zaidi sana, kama ndivyo alivyokuwa akijaribu kufanya.

62 Lakini Yusufu akiyaangalia macho yake makubwa mazuri, naye angesema, "Yusufu, Gabrieli aliniambia, 'Roho Mtakatifu

atakutia uvuli, nacho Kitu hiki kitakachozaliwa kwako—kwako ni cha Roho Mtakatifu. Ni Mungu. Hivyo ndivyo kitakavyoitwa, "Mwana wa Mungu."'" Basi, Yusufu, a—a—alitaka kuamini hilo, bali lilikuwa lisilo la kawaida kabisa. Hilo halikutukia hapo kabla.

63 Na hivyo ndivyo ilivyo tu leo hii. Laiti tungalininii tu. . .Kama ningalikuwa na njia fulani ya kuwafanya watu waone kwamba kutokuwa kwa kawaida kwa chochote, kama kimetambulishwa na Neno, basi tabia yake huthibitisha kile kilicho. Ni Mungu katika matendo.

64 Yusufu alipaswa awe analijua jambo hili. Alipaswa awe anajua, "Bikira atachukua mimba." Bali alikuwa ni mwaminifu kuhusu hilo. Hakutaka kumwacha, kwa siri, bali a—alikuwa akiwazia kufanya hivyo.

65 Na ndipo Malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto. Je! ulipata kushangaa ni kwa nini alitokea katika ndoto? Hakukuwako na manabii siku hizo. Ndoto yao ilikuwa ni rahisi sana, haikuhitaji utafsiri wowote. Kasema, "Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu mkeo, kwa maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu." Unaona, basi, hilo lilitosha. Mnaona, Yeye alimjia kwa ndoto, njia ya pili. Lakini, unaona, hapakuwapo na nabii pale wa kulitambulisha Neno hilo, kwamba, "Huyu ndiye bikira atakayechukua mimba." Mnaona? Kwa hiyo, basi, Yeye alimtokea katika ndoto, kwa maana alikuwa ni mtu mwaminifu na wa haki na mwema.

66 Nami ninaamini Mungu atamtokea mtu yeyote mwema, kwa njia fulani, na kutambulisha matendo yake kwa mtu huyo mwema, kwa ajili ya wakati, endapo mtu huyo ameitwa na Mungu kwa ajili ya wakati huo.

67 Sasa, lakini lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida sana, ilikuwa vigumu kwao kulielewa. Lakini, daima, kutokea kulingana na Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo, huku kutokuwa kwa kawaida kwote.

Sasa kuna watu wanaoweza kwenda huku na huku, na kusema, "Vema, *hili* si la kawaida, hilo ni Mungu. *Hili* si la kawaida."

68 Lakini, unaona, halina budi kutambulishwa na Neno, Nalo Neno ni Mungu. Unaona? Na kisha tabia ya utambulisho huu inatambulisha kwamba yeye ni nani, maana Mungu alisema, "*hili* lingetukia," nalo linatukia. Unaona? Tabia yake ni Neno la Mungu likitambulishwa kwa tabia ya yale yanayoendelea.

69 Yeye alisema katika siku za mwisho angemmimina Roho Mtakatifu. Akammimina. Tabia zake zilitambulisha kwamba ilikuwa ni Mungu, Neno Lake lililoahidiwa. Mnaona, daima hujitambulisha lenyewe.

70 Sasa, daima, kila wakati, husahihisha neno, wakati Neno linaponenwa kwa makosa. Mlipata kuona? Ilikuwa ni katika wakati wa Nuhu, ambao uliusahihisha wakati huo wa kisayansi, kwamba Mungu atayashusha maji kutoka mbinguni. Ilikuwa ni Musa, mnaona, aliyesahihisha wakati wote walipokuwa wametulia huko Misri, na kadhalika, lakini ilibidi Neno la Mungu kuja kutambulishwa. Nayo Kweli ya Neno hulisahihisha kosa.

71 Hebu niwaulizeni jambo fulani. Huenda tukaingia kwenye kilindi kidogo hapa. Sipaswi kuhubiri mafundisho au kanuni, bali hebu niwaulizeni tu jambo moja.

72 Yesu alikuwa ni Neno. Tunajua hilo. Biblia ilisema ndivyo ilivyokuwa. Yohana Mtakatifu, mlango wa 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Yeye angali ni Neno. Ndipo wakati alipoweza kuyatambua mawazo yao, walipaswa kujua ya kwamba huyo alikuwa ni Neno, kwa kuwa Neno la Mungu lilisema hivyo ndivyo angefanya. Yeye alikuwa ni Nabii.

73 Sasa angalia, tunaona ya kwamba hapo alipozaliwa, kwenye umri wa kama miaka kumi na miwili, alipanda kwenda kwenye sikukuu ya hema. Nao walikuwa wamepanda kwenda kwenye Pasaka. Ndipo, walipokuwa njiani wakirudi, walikuwa wameenda safari ya siku tatu nao wakamkosa; wakichukulia, wakifikiri, hasa, wakidhani kwamba Yeye alikuwa yu miongoni mwa watu wao.

74 Tungefanya somo kutokana na hilo. Hilo ni zaidi sana leo hii! Sasa enyi Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, Katoliki, chochote kile mlicho, mnaona, mnafanya jambo lile lile. Mnachukulia ati kwa kuwa Wesley alikuwa na uamsho mkuu, Luther alikuwa na uamsho mkuu, ama Pentekoste ilikuwa na uamsho mkuu, mnachukulia ya kwamba Yeye yu miongoni mwa watu, wakati, wakati mwingine hayuko.

75 Walitoka wakaenda kumtafuta. Walimpata wapi? Mahali walipomwacha, huko Yerusalemu. Na walipompata, Yeye alikuwa akifanya nini? Mvulana mdogo, umri wa miaka kumi na miwili, labda hakuwa ameingia shuleni si zaidi ya yale mama yake aliyomfundisha; naye Huyu hapa ndani ya hekalu, akihojiana na hao makuhani, juu ya Neno la Mungu. Nao walishangazwa na hekima ya Mtoto huyu. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno. Angalieni sasa.

76 Na sasa sio kutowaheshimu ninyi Wakatoliki mnaomwita Mariamu mama ya Mungu, bali hebu niwaonyeshe tu kosa dogo hapa. Endapo kanisa limejengwa juu ya Mariamu, angalieni lililotukia. Sasa yeye alikuja na akasema, "Loo, mimi na baba yako tumekutafuta, kwa machozi." Angalieni tamshi hilo, hapo

aliuhukumu ushuhuda wake mwenyewe. Alisema, “Mimi na baba Yako tumekutafuta, kwa machozi.”

77 Angalia hilo Neno. Yeye alikuwa ni Neno. Akasema, “Hamjui kwamba inanipasa kuwa kwenye shughuli za Baba Yangu?” Angalieni Neno likisahihisha kosa. Papo hapo mbele ya makuhani hao, aliuharibu ushuhuda wake. Alisema alipata mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, naye hapa alisema Yusufu alikuwa ndiye “baba” Yake. Mnaona hilo Neno likilishika upesi sana? Yeye alikuwa ni Neno. Sasa, mnajua mvulana mwenye umri wa miaka kumi na miwili asingefanya hivyo. Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ni Neno lililonenwa la wakati huo, kwa hiyo basi tabia iliyotambulishwa ya Mungu ilikuwa ndani ya Kristo. Yeye alisahihisha makosa. Akasema . . .

Hao walisema, “Mbona, sisi ni wanafunzi wa Musa.” Mnaona?

78 Akasema, “Kama mngalikuwa wanafunzi wa Musa, mngenijua Mimi. Yeye aliandika habari Zangu. Musa alisema, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.’ Mngenijua Mimi kama mlimjua Musa.”

79 Basi, mnaona, Neno daima husahihisha kosa la siku. Lakini watu hawapendi kuliamini. Wanaendelea tu, vivyo hivyo.

80 Lakini Yesu alimsahihisha mama Yake Mwenyewe. Naye mama Yake alikuwa makosani, maana tayari alikuwa amesema ya kwamba alipata mimba ya mtoto huyo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, naye huyu hapa anageuza ushuhuda wake na kusema Yusufu alikuwa ndiye “baba” yake, alikuwa ndiye baba wa—wa Yesu. Sasa ikiwa—ikiwa Yusufu . . .

81 Kama alikuwa ni mwana wa Yusufu, kama angalikuwa akifanya shughuli za baba yake, angalikuwa huko chini kwenye duka la seremala.

82 Bali alikuwa kwenye shughuli za Baba Yake, huko juu Hekaluni, akiyakemea hayo madhehebu. Mnaona? Alikuwa kwenye shughuli za Baba Yake, Mvulana tu mwenye umri wa miaka kumi na miwili. “Hamjui kwamba inanipasa kuwa kwenye shughuli za Baba Yangu?”

83 Hivi mliona wakati Yesu alipojaribiwa na Shetani? Tabia Yake pale, wakati alipokuwa kwenye kujaribiwa Kwake, ilimtambulisha kwamba ni Mungu, kwa sababu alidumu na Neno. Mnaona? “Imeandikwa,” kasema Shetani.

Yesu akasema, “Pia imeandikwa,” akadumu moja kwa moja na Neno.

84 “Mungu, zamani za kale,” tunasoma hapa, “Mungu, zamani za kale,” hiyo ni zama za kale, “njia mbalimbali,” njia nyingi, “alijitambulisha Mwenyewe kwa manabii Wake kwa maono.” Hiyo ilikuwa ndiyo tabia ya nabii, ilikuwa ni wakati alipobashiri mambo nayo yakatukia. Sasa hiyo ilikuwa ni tabia yake ya

utambulisho, kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Basi hiyo ilimpa haki ya kufasiri Neno kwa ajili ya siku hiyo, kwa sababu, "Neno la Mungu huwajia manabii," tabia ya nabii aliyobashiri.

85 Biblia ilisema, "Akitokea mtu, na analosema linatimia, basi msikilizeni; lakini, kama halitimii, msimwamini, msimwogope, bali ninii Langu. . .kama—kama Neno Langu halimo ndani yake. Lakini kama likitimia, basi Neno Langu limo ndani yake." Huo ndio utambulisho wake. Hiyo ndiyo tabia ya nabii.

86 Sasa, Mungu, zamani, hivyo ndivyo alivyoonyesha tabia Zake za utambulisho wa nafsi Yake kwa mwanadamu, kwa kunena kupitia mwanadamu aliyeitwa kuwa nabii. Sasa, Biblia inasema ya kwamba, "Mungu, zamani za kale, kwa njia mbalimbali, alisema na baba zetu kupitia manabii."

87 Vile vile tunasoma, kule kwenye Petro wa Pili, ya kwamba Neno lote la Mungu liliandikwa nao. "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliiandika Biblia." Walikuwa ni manabii. Neno lilikuja kwao nao wakaliandika, wakaliandika, chini ya uvuvio. Kwanza walikuwa ni manabii waliotambulishwa, kisha wa—wakaandika Neno la uvuvio, nao walikuwa na tafsiri ya ufunuo wa Kiungu kwa sababu ilikuwa ni Mungu katika mtu huyo.

88 Sasa hivyo ndivyo alivyojionyesha katika tabia Zake za utambulisho, maono yao yakiwa yanathibitishwa, yalikuwa ni sifa za Mungu ndani yao, akijitambulisha Mwenyewe kwa watu.

89 Sasa, hiyo ndiyo njia pekee alivyokuwa ndani ya Kristo. Nabii alikuwa tu ni chembe ndogo. Kristo alikuwa ndiye utimilifu wa Mungu. Naye Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Nazo tabia Zake zilimtambulisha, kile alichokuwa, zaidi sana hata akasema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiamini. Nisipokuwa na tabia ya Baba Yangu, basi msiniamini, msiamini madai Yangu. Ikiwa sina tabia ya Baba Yangu ndani Yangu, basi msiamini, kabisa."

90 Sasa, tabia Zake kamwe hazibadiliki. Mungu hawezi kuibadili tabia Yake, si zaidi ya—ya ninii—ya vile mwanakondoo anavyoweza kubadili tabia yake, ama kitu kingine chochote kinavyoweza kubadili tabia zake. Kwa sababu, almradi kiko kwenye asili yake, ni cha asili. Na kama ukibadilisha chochote, basi umekibadilisha kutoka kwenye asili yake.

91 Ni kama tu vile unavyoweza kumchukua ngu—nguruwe, nawe unaweza kumwosha nguruwe na—na kuyapaka rangi makucha ya vidole vyake, kama vile wanawake wafanyavyo, na kumpodoa kwa rangi za midomo, na kumvalisha nguo nzuri. Kisha umwachilie maskini huyo nguruwe jike, ataenda moja kwa moja kwenye mgaagao, na kugaagaa tena. Kwa nini? Yeye ni nguruwe, hivyo tu. Lakini, na, lakini, mwajua, usingefanya . . .

92 Mwana-kondoo asingefanya hivyo. Hata asingeingia kwenye matope hayo. Hataki chochote kuhusiana nayo. Ni tabia zake. Mnaona? Huenda ukamvisha nguo za aina hizo, bali hakika hataenda, hakika hataenda. Nje hakujalishi; ni kule ndani. Sasa, Mungu akiwa ndiye chanzo cha uhai wote . . .

93 Usikose kupata jambo hili. Ninajaribu, kwa yote yaliyo ndani yangu, kuwafanya mwone jambo fulani. Mnaona? Ni kwa manufaa yenu, enyi marafiki. Ni kwa fa—faida yenu. Mnaona?

94 Sikuja hapa nipate tu kuonekana. Sikuja hapa, ati hapakuwapo na mahali pengine pa kwenda. Nilikuja hapa kwa kuwa nilijisikia kuja hapa. Nilijisikia ya kwamba huduma ambayo Bwana alikuwa amenipa haina budi kuonyeshwa miongoni mwa watu hapa, nami ninajaribu kuwafanya mwone kile hasa Mungu alicho sasa. Yeye ni Neno Lake lililoahidiwa. Yeye daima ni Neno, Naye hujitambulisha kwa tabia aliyoahidi. Mtu fulani angeinuka katika wakati fulani, ambayo imo kwenye Neno, ndipo tabia ya mtu huyu anayepaswa kuinuka inamtambulisha kwamba ndiye mtu huyo.

95 Hiyo ndiyo sababu ilimbidi Yesu kuwa Yule ambaye alikuwa. Walipaswa kuona jambo hilo. Si ajabu walikuwa vipofu. Jambo . . . Alisema, ingawa alikuwa amefanya miujiza mingi sana, hata hivyo wasingeweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema, "Wana macho wala hawawezi kuona, na maskio wala hawawezi kusikia." Mnaona? Kila wakati, sio tu wakati Wake; bali kila wakati, jinsi gani, "Mungu, zamani za kale, kwa njia mbalimbali," bado wasingelipata.

96 Sasa, tabia zake kamwe hazishindwi. Ni zile zile daima. Sasa, kumbukeni, tabia Yake, tabia ya Mungu, haiwezi kushindwa. Kama ikishindwa, basi Mungu ameshindwa. Nayo Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, Yeye ni Mungu asiyebadilika. Tabia yoyote aliyokuwa nayo hapo mwanzo, Yeye angali ana tabia iyo hiyo. Kila njia aliyotenda kazi, wakati wowote aliopata kufanya chochote, Yeye huifanya kwa njia iyo hiyo kila wakati. Asipofanya hivyo, ni tabia Yake imebadilika, mnaona, nazo tabia Zake zingeonyesha kitu ambacho hakikuwa ni cha Mungu. Mnaona? Basi tusingejua ambapo . . .

97 Kama vile Paulo alivyosema, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejua kujiandaa kwa vita, kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana?" Sasa kama baragumu inapaswa kutoa sauti ya "rudi nyuma," hilo ndilo linalotupasa kufanya, kurudi nyuma. Kama baragumu ikitoa sauti ya "shambulia," hilo ndilo tunalopaswa kufanya, ni kushambulia. Lakini baragumu ni nini? Ni Neno la Mungu. Linamtambulisha Mungu, kama ni—kama ni "kwea, keti chini, rudi nyuma, panga silaha," chochote kile. Ni sauti ya baragumu ya Mungu.

98 Nayo sauti isiyojulikana, wakati Biblia inaposema jambo fulani linapaswa kutukia; mtu fulani anasema, “Loo, hilo lilikuwa ni la siku nyingine, hilo.” Basi kuna sauti isiyojulikana hapo. Basi hujui la kufanya.

99 Yesu alisema, “Nina uwezo wa kuutoa uhai Wangu na kuufufua tena.” Hakuna sauti isiyojulikana hapo.

100 Yule mwanamke alisema, “Tunajua yuaja Masihi; na ajapo, atatwambia mambo hayo kama Yeye alivyofanya.”

101 Akasema, “Mimi Ndimi.” Hakuna sauti isiyojulikana hapo. “Mimi Ndiye.” A-ha! Amina.

Wakasema, “Baba zetu walikula mana nyikani.”

102 Akasema, “Hao, kila mmoja wao, amekufa.” Akasema, “Lakini Mimi Ndimi Mkate wa Uzima utokao Mbinguni kwa Mungu.” Hakuna sauti isiyojulikana. “Mimi Ndimi Mti wa Uzima, kutoka kwenye bustani ya Edeni.” Hakuna, hakuna sauti isiyojulikana kuhusu hilo. Hakika hakuna. Hakuna shaka lolote kulihusu. Alikuwa na hakika katika kila alichofanya.

103 Biblia haitoi sauti isiyojulikana. Inatambulisha tabia ya Mungu katika kutoa sauti yake.

104 Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 10:37, “Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, ninii . . . na sina tabia hiyo ya Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Hizo ndizo, Zinatambulisha tabia Yake ndani Yangu, tabia Zake.”

105 Kwa sababu, Baba ni Neno, “Hapo Mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu,” nayo tabia ya Mungu inaonyeshwa na ahadi Yake ya wakati huo.

106 Sasa kama angaliishi kwenye siku za Musa, isingalifanya kazi. Na kama Musa angaliishi wakati Wake, isingalifanya kazi. Kama angaliishi katika wakati wa Nuhu, isingalifanya kazi, ama kama Nuhu angaliishi katika wakati Wake. Nuhu alikuwa akitabiri juu ya mambo ya siku hiyo, nayo tabia yake na yale aliyofanya yalimtambulisha na Neno la Mungu. Musa alifanya jambo lile lile.

107 Naye huyu hapa Yesu anakuja, na lile Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo lilitambulishwa katika Yesu Kristo kwa tabia ya Neno, ambalo ni Mungu. Amina.

108 Kumiminwa kwa Roho Mtakatifu, katika siku za mwisho, juu ya watu wa kawaida, kumeitambulisha tabia ya Mungu pamoja na watu hao. Yeye aliliahidi. Ni Neno. Alisema angefanya hivyo. Hakuna mtu anayeweza kuliondoa. Alisema angelifanya.

109 Kwa hiyo mambo haya yote ambayo ameahidi, hayo ndiyo anayofanya. Yanatambulisha tabia Yake. Naam, bwana.

"Msiamini, msiamini madai Yangu, kama tabia Yangu si ile ya Mungu."

110 Sasa angalia katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi," Yeye alisema, "yuna utambulisho Wangu, tabia Yangu. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya." Hiyo inatambulisha ya kwamba tabia ya Kristo imo ndani yake, ikionyesha tabia Yake. Amina.

111 Ninajisikia wa kidini sana sasa hivi, kama nimepwelewa na sauti. Naam, bwana. Loo, jamani! Mnaona, hakuna kosa juu Yake! Uhai Wake! "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi Yeye naye atazifanya." Mnaona, hiyo inaitambulisha ile tabia.

112 Jambo lile lile alilosema, "Kama tabia Yangu hainitambulishi Mimi, Mungu ndani—ndani Yake, basi (yeye) msimwamini." Sasa Yeye pia alisema ya kwamba angetambulishwa katika jambo hilo. Ndipo, hiyo, isipomtambulisha, basi Yeye si kile asemacho.

113 Na, leo hii, kama Kristo hajitambulishi Mwenyewe, tabia ya Kristo ikitutambulisha kwamba sisi ni wa Kristo, tukiliamini Neno . . . Yesu alikuwa ni Neno, kwa hiyo ilimbidi aliamini Neno. Nasi tunawezaje kusema ya kwamba sisi ni wa Kristo, na kukana Neno lolote la hiyo Biblia? Roho Mtakatifu wa Kristo ni Mungu ndani yako, Naye ataitikia kila ahadi kwa "Amina." Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Roho wa Mungu alisema, "Amina." Mnaona?

114 Mmoja wao hasemi, "La, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine; hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wanafunzi peke yao."

115 "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye, mahali popote ulimwenguni kote, aaminiye, ishara hizi zitafuatana naye, jambo lile lile." "Yeye yule jana, leo, na hata milele," ile tabia ikitambulishwa.

116 Hiyo inaifanya Waebrania 1:1, "Mungu wa zamani za kale, akinena na baba zetu kwa manabii," akimtambulisha Kristo, aliyefufuka leo, kwa tabia zile zile alizotambulishwa nazo zamani za kale. Je! mliona? Mungu kamwe habadilishi njia Yake.

117 Katika Biblia ya kale, wakati mwotaji alipoota ndoto, wala hapakuwapo na nabii nchini wa kuona kama ndoto hii ilikuwa ni sahihi ama siyo, walikuwa na njia nyingine ya kujua. Walimchukua mtu huyo, yeyote yule aliyeota ndoto hiyo, wakampleleka huko chini hekaluni. Ile naivera ya Haruni, aliyekuwa kuhani mkuu, ilining'inia kwenye nguzo. Basi mwotaji huyu akasimulia ndoto hii. Haijalishi ilisikika kuwa nzuri jinsi gani, jinsi ilivyosikika ni halisi; kama hapakuwapo na Nuru ya kimbinguni iliyomulika kwenye mawe hayo, ambayo inaitwa Urimu Thumimu, (wasomaji wa Biblia wanaelewa); basi, sijali jinsi ilivyosikika ni halisi, haikuwa ya kweli. Kule kutokuwa kawaida kwa Mungu, ile tabia ya Mungu, ilibidi

kuonyesha tabia Zake katika mambo ya kimbinguni, kuonyesha ya kwamba alijitambulisha Mwenyewe kwenye ujumbe huo. Amina.

118 Ninasema jambo lile lile usiku wa leo. Ile Urimu Thumimu ya kale imeondoka, lakini Neno bado ni kitu kile kile kinachoitambulisha tabia ya Mungu, ahadi ya saa tunayoishi. Hizo hapo tabia za Mungu zilizotambulishwa na ahadi ya majira tunayoishi.

119 Hiyo inamfanya Mungu kuwa sawa na jinsi alivyokuwa. "Zamani za kale," angalieni, "kwa njia mbalimbali, alisema na baba zetu kwa manabii." "Na torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana; tangu hapo, Ufalme wa Mbinguni." Angalieni, "Lakini katika siku hii ya mwisho," akinena jambo lile lile alilonena wakati huo, "kupitia Mwanawe Yesu Kristo." "Mungu, zamani za kale, njia mbalimbali, alisema na baba zetu kupitia manabii; katika siku hii ya mwisho," anafanya jambo lile lile, "akisema na watu (baba zetu) kupitia Mwanawe Kristo Yesu." Amemfufua kutoka kwa wafu, Naye anaishi ndani yetu, akijitambulisha Mwenyewe na kututabiria mambo, ya kwamba Yeye ni mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! "Mungu, zamani za kale na kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu kupitia manabii, bali katika siku hizi za mwisho kupitia Yesu Kristo Mwanawe." Maandiko hayawezi kuchezewa. Ni halisi.

120 Kama nilivyosema hapo kabla, Mungu hahitaji mtu yeyote kulifasiri Neno hili. Yeye hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Anaposema jambo lolote, linatukia, hiyo ndiyo fasiri yake. Mnaona? Hahitaji mtu yeyote kusema, "Vema, ninaamini linamaanisha *hivi*." Mungu hulitambulisha kwa tafsiri Yake Mwenyewe, Yake.

121 Kama ahadi hiyo ni kwa ajili ya siku hiyo! Hatuwezi kuishi kwenye nuru ya—ya—ya Luther. Hatuwezi kuishi kwenye nuru ya Wesley. Hatuwezi kuishi kwenye nuru ya yeyote wa hao. Inatupasa kuishi kwenye Nuru iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii.

122 Vipi kama Musa angalishuka kwenda Misri, na kusema, "Vema, tutajenga safina kubwa. Tutaelea tutoke katika nchi hii. Nile utafurika"? Wangalirejea kwenye gombo; hakuna ahadi ya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Lakini, mnaona, yeye alijitambulisha kama nabii wa Mungu, kwa kuwa yale aliyosema yalitimia, ndipo wakajua alikuwa na Neno la Bwana. Farao alikuwa na mikuki, bali Musa alikuwa na Neno. Kwa hiyo walipofika baharini, mikuki yote iliingia chini ya bahari; naye Musa akawavusha Israeli baharini, kwenye nchi kavu, kwa kuwa alikuwa na Neno, naye alikuwa ni Neno la wakati huo. Musa alikuwa Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya wakati huo.

Eliya alikuwa Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya wakati huo.

123 Kristo ni Neno lililodhihirishwa, na ahadi alizofanya. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Yeye aliahidi mambo haya. Ni kitu gani? Ni tabia ya Mungu ikilionyesha Neno Lake, kama alivyofanya katika nyakati zote.

124 Malaki 4, Yeye alisema, “Kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, tazama, nawapelekea Eliya nabii; naye atairudisha imani ya watoto iwaelekee baba zao tena, kabla siku hiyo haijaja.” Yeye aliliahidi.

125 Yesu alisema, katika mlango wa 17 wa Luka Mtakatifu, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa.” Wakati ufunuo unapojifunua, katika siku ambazo ulimwengu utakuwa kama Sodoma, itakuwa ni kitu gani? Tabia ya Maandiko hayo ikitimizwa. Mungu akijitambulisha Mwenyewe kwa tabia Yake, tabia ambazo daima amekuwa nazo. Hawezi kuziacha hizo.

126 Siku za mwisho, yeye alitambulisha kupitia Mwanawe. Angalieni jinsi ambavyo Mungu hufanya haya daima kwenye— wakati aki-. . . Kamwe habadilishi njia Yake.

127 Watu hawa watatu waliozungumza na Ibrahimu, kama vile tu tulivyokuwa tukizungumzia pale, kwenye siku za Sodoma.

128 Ibrahimu alikuwa ni mtu aliyemwamini Mungu. Aliamini ahadi ya Mungu. Sara, mkewe, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, Ibrahimu alikuwa na sabini na mitano, wakati Mungu alipomwita. Alisema watapata m—mtoto; Ibrahimu angempata mtoto kwa Sara. Huenda likasikika kidogo ni dhihaka, bali ninawazia alinunua maskini bu—buti zote na pini, na kila kitu, tayari, kwa kuwa watampata mtoto huyu.

129 Baada ya siku ishirini na nane za kwanza, mbona, huenda Ibrahimu alimwambia Sara, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hamna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, tutampata, haidhuru.”

“Wajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.”

Mwaka mmoja ukapita. “Wajisikiaje, mpenzi?”

“Hamna tofauti.”

“Tutampata, haidhuru. Mungu alisema hivyo.”

Miaka mitano ikapita. “Wajisikiaje sasa, mpenzi?”

“Hamna tofauti.”

“Tutampata, haidhuru. Mungu alisema hivyo.”

130 Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa na ahadi ya Mungu. Alimwamini Mungu, naye akatenda kama Mungu: alishikilia Neno lililoahidiwa.

131 Miaka ishirini na mitano ikapita. Buti zilikuwa tayari zimepauka, bali yeye angali alizishikilia. Sasa yeye ni mzee, na ameinama, naye yuko kwenye hali mbaya sana; nalo tumbo la uzazi la Sara lilikuwa kama lililokufa, naye mume ni mgumba. Basi ni hali ya jinsi gani waliyokuwamo!

132 "Unajisikiaje, Ibrahimu, baba wa mataifa?" marafiki wake waliojifanya waaminio wangemwambia.

133 "Vema, utukufu kwa Mungu, ninajisikia vema. Tutampata mtoto huyo, haidhuru." Kwa kuwa hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu, kwa maana alishawishika kabisa ya kwamba yale aliyosema Mungu, Mungu anaweza kuyatimiza. Amina. Hiyo hapo tabia ya mwaminio.

134 Na wewe je? Unaona? Na sisi je, watoto wa Ibrahimu? Je! tumetambulishwa na Neno la Mungu, kama ahadi, na tabia yetu inatutambulisha wenyewe, kwamba kweli tunaliamini? Ama, unasitasita tu, kuruka kutoka *hapa*, na kwenda *pale*, na *hapa* chini, na kukisia, na kusitasita huku na huku, kulihusu? Basi, sisi si Wakristo, tunajifanya tu kuamini.

135 Lakini, tukisimama kabisa kwenye ile ahadi, tuikokote pale pale na kudumu Nayo! Ibrahimu alifanya hivyo.

136 Sasa tunaona, siku moja aliona watu watatu wakija, wakitembea. Biblia ilisema hapa, "Ilikuwa mchana wakati wa jua kali," hapana shaka ilikuwa yapata adhuhuri. Watu hawa walikaribia nao walikuwa wakizungumza naye. Tunafahamu kwamba wawili wao walishuka wakaenda Sodoma. Ninaamini tulilizungumzia hivi majuzi usiku. Mmoja alibaki naye.

137 Mwangalie Mtu huyu aliyemwita. . .aliyebaki naye, kile Mtu huyo alichofanya. Mmoja alitambulikana kwa tabia Yake, kwamba alikuwa ni Elohimu.

138 Elohimu, Neno la kwanza kabisa katika Biblia, "Hapo mwanzo Mungu. . ." Sasa, yeyote wenu ninyi wanachuoni anajua ya kwamba neno *Mungu* pale linamaanisha, katika Kiebrania, ni "Elohimu," ambalo linamaanisha, "Mwenyezi, ajitoshelezaye kwa yote, anayekaa peke Yake," hahitaji msaada kutoka kwa mtu yeyote, hahitaji utafsiri wa mtu yeyote; anajitafsiria Mwenyewe. Yeye ni Mungu ajitoshelezaye kwa yote, aliye kila mahali, mwenye maarifa yote, mwenye nguvu zote. Yeye ni Mungu.

139 Huyo hapo. Naye Ibrahimu sasa, mzee huyu, aliyekuwa amelishika hilo Neno, alimtazama Jamaa huyu. Na wakati Jamaa huyu alipokuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema, Yeye alisema, "Yu wapi mkeo, Sara?"

Kasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

140 Kasema, “Nitakuzuru majira haya mwakani, nawe utampata mtoto huyu niliyekuahidi.”

141 Ndipo Sara akacheka jambo hilo. Basi Yule aliyekuwa akizungumza naye, akamwambia yale Sara aliyosema hemani, nyuma Yake.

142 Sasa, katika Mwanzo, mtasoma hilo. Tunaona ya kwamba basi, Ibrahimu, baada ya Mtu huyu kujitambulisha Mwenyewe . . .

143 Ilikuwa ni kitu gani? Waebrania, mlango wa 4, kifungu cha 12, kilisema, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, tambuzi la mawazo na makusudi ya moyo.”

144 Alijua ya kwamba huyu alikuwa ndiye yule Mtu. Alijua hakukuwako na manabii nchini ila yeye, na kwa hiyo Neno la Bwana lilikuwa limemjia. Naye alikuwa ni nabii, na hili hapa Neno likimjia nabii huyo.

145 Ni jambo lile lile kwa Yohana Mbatizaji. Hapakuwapo na nabii kwa muda wa miaka mia nne. Ninakumbuka . . .

146 Labda mzee Daktari Davis ameketi hapa, usiku wa leo, yule mhubiri mzee wa Baptisti ya Kimishenari aliyenibatiza katika Imani hii. Alizoea kubishana nami. Akasema, “Billy, wewe ni mtoto tu sasa. Inakupasa kunisikiliza.”

Nikasema, “Sawa, Ndugu Davis, ninasikiliza.”

147 Akasema, “Unaona, Yohana hakubatizwa. Kwa hiyo alikuwa akibatiza, bali yeye hakuwa amebatizwa; hakuna mtu aliyestahili kumbatiza.” Hiyo ni theolojia nzuri ya Kibaptisti. “Basi hapa akaja Yesu, na akasema basi . . . Yohana akasema, ‘Nina haja ya kubatizwa na Wewe; kwa nini Wewe waja kwangu?’ Naye akasema, ‘Kubali iwe hivyo.’” Akasema, “Basi wakati ‘alipomruhusu’,” kasema, “unaona, ndipo Yesu akambatiza Yohana. Na hapo alipotoka majini, basi mbingu zilifunguka Naye akamwona Mungu katika umbo la hua, akishuka chini na kumwendea juu yake, kasema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.’” Lakini, la, sio kutokukubaliana na Daktari Davis, bali alikosea.

148 Unaona, Yohana alikuwa nabii, nalo Neno daima humjia nabii. Kwa hiyo kama Neno lilifanyika mwili, ilibidi limjie nabii, kwa vyovyote vile; maana, alikuwa akilishuhudia Neno, na tabia yake hasa ilimtambulisha Yeye hivyo. Huyu hapa Neno anakuja, sasa kulitokea nini? Mara tu alipoenda mbele ya Yesu, Yohana alisema, “Nina haja kubatizwa na Wewe; kwa nini Wewe waja kwangu?”

149 Yesu akasema, “Kubali iwe hivyo, kwa kuwa imetupasa (tunapaswa) kutimiza haki yote.” Yohana akiwa ni nabii; Yeye akiwa ni Neno. Yeye alikuwa ndiye Dhabihu, Naye alikuwa akijiandaa kuingia kwenye huduma Yake ya duniani,

nayo dhabihu ilibidi ioshwe kabla haijatolewa. Basi Yohana akambatiza, maana alijua. "Kubali iwe hivyo, kwa kuwa imetupasa kutimiza haki yote." Dhabihu ilibidi kuoshwa kabla haijatolewa, na kwa hiyo Yohana akambatiza. Haikuwa Yesu akimbatiza Yohana. Yohana alimbatiza Yesu. "Kubali iwe hivyo."

150 Angalia, huyu hapa Ibrahimu, naye alikuwa na Neno la Bwana. Neno la Bwana lilimjia. Alikuwa ni nabii. Na sasa hili hapa Neno linakuja. Yeye alimwita, "Ibrahimu," sio *Abramu*.

151 Siku chache kabla ya hapo, jina lake lilikuwa Abramu—lilikuwa Abramu, sasa ni Ibrahimu. Mkewe alikuwa Sarai, sasa ni "Sara," sio S-a-r-r-a; S-a-r-a. Sio (I-b-r-a-h-i-m-u) A-b-r-a-m-u, bali I-b-r-a-h-i-m-u, Ibrahimu.

152 Naye mtu huyu akajitambulisha Mwenyewe, wakati aliposema, "Ibrahimu!" Loo, jamani!

Ibrahimu akasema, "Elohimu!"

153 Hilo hapo Neno na nabii, pamoja, wote wawili wametambulishwa.

154 Elohimu, Yeye akasema, "Yu wapi mkeo, Sara?"

155 Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako." Ndipo ninii... Basi mwujiza ukafanyika. Elohimu! Ibrahimu alimwita, "ajitoshelezaye kwa yote, Mwenyezi, Mungu mwenye nguvu zote."

156 Yesu alisema, wakati alipokuwa duniani, alifanya jambo lile lile Elohimu alilofanya. Hiyo ilitambulisha tabia Yake kwamba ni Mungu.

157 Na Yeye alisema, hapo kabla, "Katika siku za mwisho, wakati tu wa kuja kwa Mwana wa Adamu, wakati anapofunuliwa, hali hii itatukia tena, kama ilivyokuwa Sodoma." Elohimu miongoni mwa watu Wake, Mungu Mwenyezi! Hilo ndilo Maandiko yasemalo. Elohimu miongoni mwa watu!

158 Kwa miaka arobaini Yeye amekuwa akitubatiza kwa Roho Mtakatifu, Elohimu, Mungu! Nalo kanisa...

159 Angalieni, Ibrahimu aliona ishara moja, wito mwingine; ishara, wito; wito, ishara; akimngojea yule mwana aliyeahidiwa. Lakini ishara ya mwisho aliyoona, kule kuonekana kwa mwisho, kutembelewa kwa mwisho na Mungu kabla ya mwana aliyeahidiwa kuwasili jukwaani, ilikuwa ni Elohimu katika mwili wa kibinadamu. Ndipo mwana aliyeahidiwa akaja.

160 Nao Uzao wa Ibrahimu unamngojea Mwana aliyeahidiwa, Yesu Kristo. Nao wameziona ishara, kumiminwa kwa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, uponyaji wa Kiungu, na kadhalika. Lakini wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa, Elohimu atarudi kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu na

kuonyesha jambo lile lile aliloonyesha kwenye siku ile, amina, Elohimu, kama ilivyokuwa! Kwa nini? Itakuwa ni tabia ya Mungu.

161 Sasa, kama Kristo alikuwa ni Mungu, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari, ule mwisho. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

162 Yesu alisema hayo katika—katika Luka mlango wa 17. Vema, tunapoamini na kuziona siku hizi za mwisho, hali hii yafaa kurudiwa tena.

163 Kwa hiyo, Waebrania 1:1, "Mungu, zamani alijitambulisha Mwenyewe kupitia manabii, katika siku hizi za mwisho ameutambulisha ufufuo wa Mwanawe kutoka katika wafu," kwa kulipa Kanisa tabia ile ile aliyokuwa nayo, akiifanya Waebrania 13:8 kweli kabisa.

164 Hakuna manyoya yanayoweza kung'olewa humo. Hayo ni manyoya ya tai. Yameshika kabisa, kwa maana ni ndege wa kimbinguni. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... wanawalisha chakula cha tai.

165 Sasa tunaona ya kwamba, "Zama za kale, kwa njia mbalimbali, Yeye alisema na baba zetu kwa manabii, katika siku za mwisho kwa Mwanawe Yesu Kristo, kwa kumfufua kutoka katika wafu." Naye huyu hapa miongoni mwetu, baada ya miaka elfu mbili, Yesu yeye yule, sio mmoja wa wanabii; Yesu, haleluya, Mwana wa Mungu aliyefufuka!

166 Yesu alisema, siku moja, Yeye alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara, nao watapata ishara." Kizazi kiovu na cha zinaa. Ni wakati gani ulimwengu ulipata kuwa mwovu zaidi, ama uzinzi na kupotoka, kuliko ulivyo sasa?

167 "Kama ilivyokuwa katika siku za Yona, kama Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku."

168 Basi, "kizazi kiovu na cha zinaa" kilikuwa kipokee ishara. Ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo. Nasi tunayo leo hii, baada ya miaka elfu mbili, Yeye angali hai. Yuko miongoni mwetu, usiku wa leo, yeye yule jana, leo, na hata milele, akijitambulisha Mwenyewe kwa tabia za Mungu, akilidhihirisha Neno katika siku hii ya mwisho aliloahidi kufanya. Amina.

169 Hilo hapo Neno. Sasa je! mtaiamini ishara, ndilo jambo linalofuata, siku za mwisho, utambulisho Wake kwa Mwanawe? Angalieni.

170 Mungu alinena na Musa zamani za kale. Katika Kumbukumbu la Torati 18:15, inasema, "Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi." Sasa angalieni.

Hilo ni Neno. Hilo ni Neno. Huyo alikuwa ni Mungu. Huyo hakuwa ni Musa. Musa angejuaje hilo; akiwa ni mwanadamu? Bali Mungu, akinena kupitia Musa, alisema hili. Mnaamini hilo? Vema.

171 Sasa angalieni Yesu, angalieni jinsi tabia Za—Zake zilivyolitambulisha Neno hili lililoahidiwa kwamba ni kweli. Hakika alilitambulisha. Alitambulishwa na tabia hii ambayo Musa alisema angekuwa.

172 Wengi wao, kama ilivyo leo, wanataka kumwona kiongozi fulani mkuu. "Loo, huyu ni Daktari Ph. *Nanii wa nanii*. Ametoka Chuo Kikuu cha Hartford. Ama, ametoka kwenye baadhi ya mahali fulani pakubwa namna hiyo." Huo si utambulisho wa Mungu. La, la. Hakuna kitu kuhusu hilo. Neno ndilo linalomtambulisha Mungu. Mnaona?

173 Yesu hakuwa msomi, wala hakuwa kuhani, wala hakuwa rabi, kwa ulimwengu. Alikuwa ni haini, kwa ulimwengu.

174 Lakini Mungu alikuwa akilithibitisha Neno Lake kupitia Yeye, ambalo lilimfanya Imanueli. Huo ulikuwa ndio utambulisho Wake. Sasa, hapa, Yesu akitimiza hili ambalo Mungu zamani za kale alisema Yeye angefanya, kupitia Musa, yale angefanya.

175 Sasa angalieni hapo alipokutana na Petro, kama tulivyolielezea kidrama hivi majuzi usiku, hapo alipokutana na Petro na kumwambia Petro jina lake lilikuwa ni nani. Ishara hii iliyatambulisha madai Yake ya Umasihi, kwa Petro, kwa kuwa Neno lilikuwa limesema, "Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii."

176 Ndipo Petro akaja, ambaye alikuwa Simoni wakati huo, akakwea hata mahali Yeye alipokuwa. Ndipo Yesu akamwangalia, kasema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo liliitambulisha tabia ya Kristo kuwa ni lile Neno ambalo Musa aliahidi. Petro alitambua ya kwamba ishara hiyo ilimtambulisha Yesu kama Masihi. "Mungu alikuwa katika Kristo," upako kwa ajili ya siku za mwisho. Kwa Nathanaeli . . . Kumbukeni, alimwambia Simoni jina lake.

177 Sasa, angalieni, kwa Nathanaeli Yeye alimwambia yale aliyokuwa amefanya. "Ulikuwa chini ya mtini nilipokuona." Hilo lilimtambulisha kama Masihi.

178 Kasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli." Alitambulishwa kwa tabia ya Neno lililoahidiwa kwamba alikuwa awe ndiye Masihi. "Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii."

179 Maskini yule mwanamke kisimani, Yeye alimwambia kile alichokuwa, na hilo likamtambulisha kama Masihi huyu aliyeahidiwa. Mnaona?

180 Tabia Yake, tabia Zake, zilikuwa ni Neno likitambulishwa. Ilikuwa ni tabia Zake zikionyesha kwamba Neno ni Mungu, kwa hiyo huyo alikuwa ni Mungu akitambulishwa ndani ya Kristo. Sasa liangalieni. Tazameni.

181 Kwa Petro, Yeye alitambulishwa kwa Petro kwa kuliita jina lake. Alitambulishwa kwa Nathanaeli kwa kumwambia kile alichokuwa amefanya. Alitambuliwa na yule mwanamke, kwa kumwambia kile alichokuwa. Kile yeye. . . kwamba *yeye* alikuwa ni nani; yale *aliyofanya*; na kile *yeye* alichokuwa. Alitambulisha tabia Yake ya Kimasihi ambayo ilikuwa iwe ndiyo tabia ya Masihi.

182 Mwangalieni maskini mwanamke yule akisema jambo lile lile. "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Tumekuwa na wingi wa makanisa, misukosuko mingi na tofauti za kimadhehebu, bali hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Tunajua ya kwamba atakapokuja Masihi, hili ndilo litakalomtambulisha."

183 Akasema, "Mimi Ndiye, ninayesema nawe." Hakuna tashwishi juu yake, "Mimi Ndiye." Hilo lilimtambulisha.

184 Yule mwanamke mwenye kutokwa na damu, alimtambua kama Neno. Vipi? Kwa yale aliyofanya wakati imani yake ilipomgusa. Aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Alijua jambo fulani lilitukia. Hilo lilimtambulisha Yesu kama Masihi.

185 Aliliamini, naye akasema, "Kama ninaweza kugusa vazi Lake, nitaponywa."

186 Kwa hiyo mara tu alipogusa, Yeye aligeuka, kasema, "Sasa, ni nani aliyenigusa?" Nao wote wakakana. Lakini tabia Yake ya Kimasihi . . .

187 Amina! Ninatumaini mnaona jambo hilo, enyi kusanyiko. Sikilizeni, tunapofunga.

188 Hapo akamgusa. Kulikuwako na mamia, labda, wakijaribu kumgusa. Petro hata alimkemea, kasema, "Vema, wote wanakugusa."

189 Akasema, "Naam, ila mtu fulani amenigusa isivyo kawaida." Hiyo ndiyo tofauti yake, huo mguso wa imani. Mnaona? Kasema, "Mtu fulani alinigusa. Ulikuwa ni mguso tofauti. Nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka. Uweza umenitoka." Sasa, huyo hapo amesimama.

190 Sasa, hata mwanafunzi Wake Mwenyewe akisema, kwa maneno mengine, "Unasikika—unasikika kana kwamba ulikuwa mtu mwenye kasoro. Mbona, watu, kila mtu anakugusa."

191 Angalieni ninii Yake, angalieni utambulisho wake sasa. Aligeuka, akaangalia kwenye umati. Akamtenganisha moja kwa moja. Asingeweza kujificha tena. Akamwambia kuhusu hali yake, na kusema, "Imani yake ilikuwa imemponya."

192 Alijua kwa jambo hili, ya kwamba, Waebrania 4:12, “Neno huyatambua mawazo, makusudi ya moyo.” Tabia Yake ilimtambulisha kuwa “Neno la Mungu lililofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu.” Amina.

193 Nafikiri jambo lile lile usiku wa leo linamtambulisha, Yesu Kristo aliyefufuka akiishi miongoni mwetu usiku wa leo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, kwa kuwa Waebrania 13:8 ni ya kweli, tabia Yake itamtambulisha leo hii, kama ilivyofanya wakati huo, vivyo hivyo.

194 Mwangalieni Kleopa na hao wengine, baada ya ufufuo. Yesu alijitambulisha Mwenyewe kwa jinsi alivyoumega ule mkate, kwamba alifanya kama alivyofanya kabla hajasulibishwa. Nao. . .Hilo liliitambulisha tabia Yake, maana hivyo ndivyo alivyolifanya.

195 Sasa kama alikuwa hapa usiku wa leo, angejitambulishaje? Kama tu alivyofanya jana, kwa maana ni yeye yule leo, na atakuwa milele. Ni utambulisho. Waebrania 4, -nne. . . 14 na 15, “Yeye sasa . . . ” Inasema, “Yeye ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Yeye ni Kuhani wetu Mkuu sasa hivi. Baada ya kufufuka Kwake, baada ya kifo Chake, baada ya kuzikwa Kwake, baada ya kufufuka Kwake, baada ya kupaa Kwake, amina, angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu. Amina. Ndivyo alivyo, sasa hivi, kwa kila mwanamume na mwanamke hapa atakayeamini hilo. Yeye ni Kuhani wetu Mkuu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

196 Yu hai daima. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.] Tabia Zake zinaendelea kumtambulisha ni yeye yule kama alivyokuwa wakati alipoishi duniani. Angali anaishi hapa, usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu. Yu hai daima. Nazo tabia zake zinamfuata, kama tu vile zilivyofanya daima, kama yungali hai.

197 Nina shukrani, usiku wa leo, kwamba, “Mungu, zamani za kale na kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu kupitia manabii, katika siku hizi za mwisho kupitia Mwanawe Yesu Kristo.”

198 Jamani, sikujua nilizungumza kwa muda mrefu hivyo. Nilisahau kwamba ndivyo ilivyo. Samahani. Nitaninii tu. . . Nitaacha.

Na tuombe.

199 Baba wa Mbinguni, Mungu mkuu mwenye rehema! Bwana, mimi—mimi. . .labda mimi hunena kupita kiasi. Ninaomba, Mungu, kama nilifanya hivyo, naomba unisamehe. Lakini, Bwana, siwezi kuomba msamaha kwa yale niliyosema. Nilisema tu yale uliyosema katika Neno Lako hapa.

200 Sasa neno moja tu ama mawili kutoka Kwako, Bwana, labda kila mtu hapa ataliona usiku wa leo. Maskini, watu wagonjwa wataponywa watakapoona ya kwamba ungali ni Kuhani wetu Mkuu. Ninaomba, Bwana, katika dakika hizi chache zinazofuata, kwamba utaufanya Ujumbe huu uishi tena katika uhalisi. Kwa yale niliyosema kwa Neno, jalia tabia yako ikutambulishe miongoni mwetu, usiku wa leo, kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa kuwa ni katika Jina la Yesu tunaomba hayo. Amina.

201 Hebu kidogo sasa. Sisi, kidogo ni—nimechelewa, lakini ninyi nyote mwaweza kuvumilia muda kidogo kutosha kufanya mstari mdogo wa maombi kwa dakika kumi na tano, ishirini? Ikiwa utavumilia, inua mkono wako, useme, "Tutaninii . . ." Vema, asante—asanteni. Niliahidi kuwaachilia saa tatu u nusu. Ni wakati huo sasa; zimesalia dakika ishirini. Kwa hiyo kama mtanipa tu kama dakika kumi, nitaharakisha moja kwa moja.

202 Hebu tuone, walisambaza kadi gani za maombi leo? [Ndugu mmoja anasema, "O."—Mh.] O? Nini, tulianzia wapi hivi majuzi usiku, moja, moja? ["Nafikiri ilikuwa ni moja."] Naam, a-ha.

203 Halafu basi sisi, jana usiku, tulininii tu . . . Roho Mtakatifu . . . Nilikuwa nikisikiliza leo hii, na kurudia yaliyosemwa. Baadhi ya hayo majina ya Kifaransa, nilikuwa . . . Roho Mtakatifu; njia pekee ningaliweza kufanya hivyo, kungoja tu na kuona.

204 Mnaona, wakati mwingine unapoona ono, halina budi kugeuzwa na kufasiriwa. Linafasiriwa. Ono, kama vile unge—ungeona ko—kondoo, hiyo inaweza kumaanisha sufu. Mnaona, inakubidi kuwa pia na tafsiri yake, unaona, na kuligeuza ono hilo na kulifasiri.

205 Nami niliona jana usiku, ni—nisingeweza kuyatamka majina hayo ya Kifaransa, ilinibidi kutaja tahajia zake.

206 Huko Afrika na kwa hao Wahotentoti na makafiri, na kadhalika, ingembidi kutaja tahajia za majina yao moja kwa moja, kuwaambia kuwa wao ni akina nani, kutaja tahajia zao moja kwa moja katika lugha zao. Wao, wao wangejua ilikuwa ni nini, mara tu ulipozitaja tahajia hizo. Lakini, mnaona, bali Yeye anazijua lugha zote. Yeye ni Mungu wa Milele.

207 Hebu tuanze usiku wa leo kwenye, hebu tuseme, sabini na tano, hadi mia moja, katika O. Ni O, hivyo ndivyo alivyosema? Mimi . . . [Ndugu fulani anasema, "Naam, O."] O, O. Naam. Vema. Ni nani aliye na kadi ya maombi sabini na tano, hebu tuione? Katika O, kadi ya maombi O, sabini na tano, inua mkono wako, yeyote aliye nayo. Ma-O. Vema. Njoo moja kwa moja *huku*. Sabini na tano, themanini, themanini na tano, tisini, tisini na tano, mia moja, njoo *huku* ukiweza.Vema, ni, pangeni mstari moja kwa moja huku, upesi sana, maana hatutakuwa na wakati. Nitatumaini tu kwamba mtafanya hivyo.

208 Angalia kadi yako ya maombi. Angalia kadi ya maombi ya jirani yako. Ni ninii jinsi gani . . . Na iwapo mtu fulani ni kiwete, waleteni moja kwa moja kwenye mstari wa maombi. Kwa hiyo kama wana O, kama tu O, sabini na- . . .

209 Sabini na tano hadi mia moja, fanyeni mstari *hapa*, tafadhalini. Popote ulipo, kwenye roshani, popote pale, shuka moja kwa moja, na uje mstarini upesi iwezekanavyo, tafadhali, ili kuokoa wakati.

210 Sasa ninyi wengine hapa, msio na kadi ya maombi, mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, "Sina kadi ya maombi, Ndugu Branham, bali ninaamini"? Inueni mikono yenu.

211 Sasa kumbukeni, nitazungumza nanyi kuhusu yule Kuhani Mkuu. "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu." Yeye ni *Yehova-Yire*, "Dhabihu ya Bwana iliyotolewa." Yeye ni *Yehova-Rafa*, "Bwana ayaponyaye magonjwa yenu yote." Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina.—Mh.] Yeye ni *Yehova-Manase*. *Kinga*, *ngao*, *amani* yetu, angali hivyo. Vema, ni wangapi wanaoamini ya kwamba majina hayo yote ya ukombozi ya Yehova yalitumika kwa Yesu? ["Amina."—Mh.] Hakika, ilibidi awe hivyo. Kama Yeye—kama Yeye . . . Mbona, hawatengeki, kwa hiyo ilibidi awe hayo yote. Na kama angali ni Yehova-Yire, Yeye ni Yehova-Rafa. Kama Yeye ni Yehova-Yire . . . Yeye ni *Yehova-Yire*, ni "Dhabihu ya Bwana iliyotolewa kwa ajili ya wokovu," basi Yeye ni *Yehova-Rafa* ambaye "huyaponya magonjwa yetu yote." Amina. Uponyaji unaweza tu kutokana na Mungu.

212 Vema, wakati watu wakipanga mstari; sina muda wa kuona hao ni akina nani na jinsi walivyo. Lakini sasa, ninyi nyote huko mnaojua ya kwamba siwajui, inua mkono wako, useme, "Nina haja na Mungu. Lakini hunijui, Ndugu Branham, bali nina haja na Mungu. Nitauinua tu mkono wangu."

213 Sasa kama mtatulia tu kwa dakika chache, mwangalie, iweni waangalifu, nyamazeni. Sasa simaanishi, ninaposema, "nyamazeni." . . . Kama Bwana akitenda jambo lolote, utapenda kumsifu Bwana; huko ni kuabudu. Lakini ninalomaanisha, "kukimbia tu huku na huku, kusimama," mwajua, huko ni kutokuwa na kicho. Mnaona? Naye Roho Mtakatifu ni mwoga sana, mwoga sana. Mnaona? Kitu tu chochote kama hicho, ananiacha tu, nami sina budi kupiga vita basi, tena, mnaona. Lakini laiti mngalisikiliza tu!

214 Mnaikumbuka ahadi yake ya kwanza? "Ukiwafanya watu wakuamini, na kisha uwe mwaminifu, hakuna kitakachosimama mbele ya maombi." Mnakumbuka hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Na hiyo ni . . . Sijaiona ikishindwa bado, wala haitashindwa. Ni Mungu.

215 Sasa tutauharakisha mstari wa maombi, kusudi tuwapishe wengi tuwezavyo, kwa ajili ya watu. Lakini ninyi mlio na kadi

za maombi na hamkuitwa usiku wa leo, shikilia kadi yako, tutawafikia. Vema.

216 Sasa ninyi huko nje msio na kadi za maombi, kumbukeni. Ama, ninyi huko nje, kama mna kadi za maombi ama hamna, aminini tu kwamba Yeye ni kama Waebrania mlango wa 4 hapa. “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuliana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Angalieni kama Yeye angali. . .Angalieni kama Yehova amejiwakilisha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, kama alivyofanya katika siku za Sodoma. Vema.

217 Vema, bwana. Sasa hebu tuombe, sasa, iweni na kicho kabisa. Sasa kumbukeni, neno moja kutoka kwa Mungu ni zaidi ya yale mtu yeyote angaliweza kusema. Sasa, mtu huyu hapa, si—simjui. Nami nafikiri yeye ni. . .Wewe ni mgeni kwangu, sivyo, bwana? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] U mgeni. Tunajua jambo moja, ya kwamba sote wawili hatuna budi kusimama Mbele za Mungu siku moja; kama wanadamu, hatuna budi kukutana Kule. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana.

218 Sasa kama ukija hapa, kama wewe ni mgonjwa, sijui; huenda ikawa ni jambo lingine, unaona. Lakini kama ningalininii—kama ningalikuwekea mikono, niseme, “Bwana asifiwe! Nenda zako, uwe mzima.” Hilo ni sawa. Ungeweza kuamini hilo. Lakini vipi kama akikwambia shida yako ni nini? Sasa, unaona, hiyo ni tofauti, basi unajua hilo linaitambulisha tabia Yake. Unaona, hiyo isingekuwa ni tabia yangu. Mimi ni mwanadamu; nisingejua lolote kumhusu. Nilimwambia tu, “Sikujui mimi.” Hanijui. Lakini hilo lingefanya nini? Hilo lingeitambulisha tabia ya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Ukijua ya kwamba isingewezekana kuwa ni mimi, isingewezekana kuwa ni mimi, maana simjui mtu huyu. Nitainua mkono wangu; *hili* hapa Neno. Mnaona? Simjui. Hanijui. Bali tabia ya Yesu Kristo . . .

219 Kama Yesu alikuwa amesimama hapa; naye ni mgonjwa. Kama angesema, “Bwana Yesu, niponye.” Yesu angemwambia nini? “Nimekuponya tayari.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina”.—Mh.]

220 “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa mapigo Yake tuliponywa.” Ukombozi wote tunaoweza kuupata ulimalizwa pale Kalvari. Tangu hapo na kuendelea, ni imani, kuamini kazi iliyomalizika. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

221 Sasa, sasa kama Yesu yu hai, nami nimezungumza juu ya Neno Lake. . .Haya basi, turejee kwenye urahisi huo na imani, tukiliamini Neno Lake. Wakati alipokutana nami usiku ule, Yeye alisema, “Itakuwa kwamba hata utajua siri za moyo wao. Wasipoiamini ishara hiyo ya kwanza ya mkono, itawabidi kuamini hii. Mnaona? Wasipofanya hivyo, basi damu itailaani nchi.”

222 Kama tu ilivyofanya katika wakati wa Musa. Kasema, "Wasipoamini hizo ishara mbili, basi imwage damu juu ya nchi. Mnaona, mwaga maji juu ya nchi, yatakuwa damu."

223 Sasa kutafuta tu kujua. Kama ninaweza tu kuona shida yako ni nini, hilo litakuridhisha na kukufanya uamini, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Hakika."—Mh.] Unajua itabidi iwe ni tabia ya Mtu yule ninayenena habari Zake, Yesu Kristo.

224 Mtu huyo, huku nikimwangalia tu, anarudi nyuma. Ametiwa uvuli. Hakuna kitu ambacho dawa zingeweza kumsaidia mtu huyu. Yeye yuko katika hali ya kufa. Hiyo ni kweli. Amekuwa na upasuaji, nao upasuaji huo ulikuwa ni upasuaji wa tezi kibofu. Nayo ni kansa, nayo hiyo kansa imetapakaa mwilini mwako mwote. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mungu pekee ndiye anayeweza kumponya. [Ndugu huyo anasema, "Haleluya! Haleluya! Haleluya!"—Mh.] Lakini, angalia, ninataka kukwambia jambo fulani, bwana. Ibilisi huyo huenda alijificha kutoka kwa kisu cha daktari, bali hawezi kujificha kutoka kwa Mungu. Unaamini hilo? Unaliamini? ["Loo! Loo!"] Basi naomba, kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kitu hicho na kimwache, mtu huyu na aishi. Hamna kitu; ni kuwa tu dhaifu. Vema.

225 Mimi na wewe hatufahamiani, mwanamume na mwanamke wanakutana. Sasa, kama mwanamume, sikujui. Na labda, kama mwanamke, hunijui mimi; si zaidi ya vile umeliona tu jina langu, ama picha, ama kitu kama hicho. Bali hatufahamiani. Hizo ni tabia zetu. Hatujui tabia za mmoja kwa mwingine. Lakini tabia ya Kristo, Yeye ni Neno, nalo Neno limeahidiwa kwa ajili ya siku hii. Ulinisikia nikinena habari zake. Basi tabia Zake zingemtambulisha Yeye hapa. Sio mimi kumtambulisha. Sikujui mimi. Unaelewa. Je! kusanyiko le—letu linaelewa hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Mimi—mimi ni mwanadamu. Mimi ni ndugu yako tu.

226 Kama vile yule mwanamke kisimani, aseme jambo fulani lililo kasoro, una kasoro fulani, ama kile unachohitaji, ama kilichokuleta hapa. Acha Mungu awe hakimu wa hayo. Unaugua ugonjwa wa anemia. Hiyo ni kweli, sivyo? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.]

227 Da—daima ninagongana na hilo, mtu fulani akifikiri nililibahatisha. Sibahatishi hilo. La. Mara moja moja, ninahisi hilo, mtu fulani. Huwezi kuyaficha mawazo yako sasa. Sasa kuna yapata, najua, wenye kushuku wawili wabaya sana wanaoketi hapa. Mnaona? Basi sasa kumbuka ninaweza kulitaja jina lako, vilevile, Mungu anaweza, kwa hiyo ninyi acheni kuwazia hilo. Hebu niwaonyeshe.

228 Angalia hapa, mama. Niangalie mimi. Sijui yale aliyokwambia, bali na—najua Yeye ni nini. Na hiyo ni tabia

Yake iliyotambulishwa. Naam, ni ugonjwa wa anemia, damu, maji.

229 Sasa, hapa, hili hapa jambo fulani. Angalieni kama wanawazia huku ni kubahatisha. Una mtoto unayemwombea, ambaye yupo hapa. [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Hiyo ni kweli. Anayo katika koo lake, ["Ndiyo."], mafindo, vichukulia vya limfu. Amepangiwa upasuaji. Si ni kweli? ["Ndiyo."] Chukua leso hiyo ukaiweke juu yake, na uamini. ["Ndiyo."] Usitie shaka. Hatahitaji upasuaji. Sasa amini kwa moyo wako wote.

230 U hali gani? Jambo ni kwamba, kwa mwanamke huyu hapa, kwamba unahofia jambo fulani. Unahofu kwamba alama ya kuzaliwa imegeuka ikawa kansa. [Dada huyo analia kwa sauti kuu, "Loo!"—Mh.] Sasa nenda zako, ukiamini, na haitakuwa hivyo. Nenda zako tu, ukiamini kwa moyo wako wote. Tabia, sio zangu; Zake.

231 Mnaamini sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hilo linapaswa kumfanya kila mtu aamini. ["Amina!"]

232 Sasa, sikujui wewe. Mimi ni mgeni kwako. Mungu anakujua. Unaamini hilo? Unajua ya kwamba sikujui, nawe unajua hunijui, kwa hiyo je! unaamini ya kwamba Roho hii inayonena haiwezi kuwa ni roho yangu? Kwa sababu, mimi, kama mwanadamu, sikujui. Lakini tabia ya Neno lililoahidiwa ni Neno ambalo ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

233 Wewe ni mgonjwa sana. Ulikuwa na tatizo la wanawake, ambalo lilikuwa ni tumbo la uzazi, na tumbo hilo lilikuwa na kansa. Nawe uliondoka ukaenda ukapata matibabu ya namna fulani, yalikuwa ni matibabu ya radiamu, na jambo pekee yaliyofanya ni kulisambaza mwilini mwako mwote. Nawe uta—utakufa Mungu asipokuponya. Hiyo ni kweli. Je! unaamini sasa Yeye atakuponya? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Mungu wa Mbinguni na amkemee pepo huyo ambaye amejificha kutoka kwa daktari. ["Loo!"] Huenda alijificha kutoka kwa radiamu, bali si kwa Roho Mtakatifu. Nenda zako, mwamini Yeye, sasa, dada. Usitilie shaka hata kidogo, bali amini. ["Ee Mungu, niponye!"]

234 Unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa pumu, na kukufanya mzima? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Unaamini? Basi nenda zako, ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana. Ninaamini pumu yangu imekwisha."

235 U hali gani? Una wasiwasi. Umekuwa na wasiwasi kwa muda mrefu. Mle ndani, imesababisha donda la mmeng'enyo kuingia tumboni mwako, ambalo linakufanya—linafanya tumbo lako lisumbue. Nawe unataka . . . Je! unataka kula chakula chako cha jioni? Je! utafanya kile nitakachokwambia ufanye? Nenda zako, ukale, katika Jina la Bwana Yesu.

236 Unaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Wewe ni msichana mzuri sana, inavyoonekana. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? ["Amina."] Unaamini tabia Yake ingeweza kuwa hapa, pia, Neno, Lenyewe, na ahadi ya siku hii, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya"? ["Amina."] Siwezi kuponya. Tayari amefanya hivyo; bali tabia Yake humwonyesha, inaweza kujua shida yako. Una tatizo la wanawake, tatizo la kike. ["Ndiyo, bwana."] Je! unaamini kwamba Mungu analiponya sasa? ["Ndiyo. Amina."] Nenda zako, halitakusumbua tena. Amini kwa moyo wako wote.

237 Unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaamini ni tabia ya Yesu Kristo? Iko mgongoni mwako. Haiko tena. Nenda, amini kwa moyo wako wote. Amini.

238 Njoo, mama. Wewe pia una ugonjwa wa tumbo. Amini kwa moyo wako wote, kisha uende ukale chakula chako cha jioni. Isahau. Yesu Kristo anakuponya.

239 Njoo. Shida yako ni damu yako. Una kisukari. Unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya na kukuponya huo? Nenda zako, na useme, "Asante, Bwana Yesu," anakuponya. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

240 Njoo. Mgongo wako, unaamini Mungu atauponya mgongo huo na kukupa afya? Nenda zako, na ushangilie, na kusema, "Asante, Bwana Yesu."

241 Wewe pia ulikuwa na tatizo fulani mgongoni mwako. Endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana. Nimeponywa." Amini kwa moyo wako wote.

242 Wewe pia ulikuwa na tatizo la mgongo. Unajua nini juu ya huo? Amini kwa moyo wako wote sasa, kisha uende zako ukapate afya. Amini Yesu Kristo anakufanya mzima. "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Vema.

243 Vipi kama sikusema lolote kwako; nilipita tu na kumwekea mkono, mnaamini angepona? Wanaona shida yake. Mnaamini angepona? Njoo hapa. Ninamchukia ibilisi huyu, katika Jina la Yesu Kristo. Nguvu za Mungu na zimponye mtoto huyu. Amina. Usitilie shaka, usitilie shaka hata kidogo, naye atapona. Amini kwa moyo wako wote.

244 Mungu asipokuponya, utatembea kwa mkongojo siku moja, kwa yabisi kavu. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anaponya yabisi kavu yako? Basi nenda zako, ukisema, "Asante, Bwana. Nitakuamini, na Wewe unipe afya." Vema.

245 Njoo sasa. Kweli ni umri wako. Una wasiwasi kweli. Unashikwa na wasiwasi sana, jioni sana. Unapofanya kazi na kadhalika, unashikwa na wasiwasi kabisa. Unaamini sasa?

Basi hautakusumbua tena. Nenda zako, ukisema, "Asante, Bwana Yesu."

246 Njoo, bwana. Unaamini ya kwamba Mungu huponya matatatizo ya moyo? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Atauponya moyo wako? Endelea tu kusonga mbele, ukisema, "Asante, Bwana. Ninaamini kwa moyo wangu wote."

247 Mungu huponya TB, na kukupa afya, pia. Unaamini hilo, bwana, kwa moyo wako wote? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Vema. Nenda zako huku ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana Yesu."

248 Vipi ninyi mlio huko nje, mnaamini? Vipi kuhusu wasikilizaji? Baadhi yenu katika wasikilizaji sasa aminini.

249 Mtu huyu anayeketi papa hapa, akiwa na mkamba, unaamini Mungu atauponya ugonjwa huo wa mkamba? Vema, unaweza kupata ulichoomba, basi. Amina.

250 Shinikizo kuu la damu, unayeketi moja kwa moja nyuma yake hapo. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya shinikizo lako kuu la damu? Lilikuacha, bwana. Simjui, sijapata kumwona maishani mwangu.

251 Aisee, bwana, unaamini ya kwamba mishtuko hiyo kwenye misuli yako, mishtuko ya neva za misuli, unaamini Mungu ataiponya? Unaamini? Inua mkono wako kama unaamini. Vema.

252 Mke wako anayeketi hapo, anasumbuliwa na ugonjwa wa mapindi. Unaamini utakuacha, pia, dada?

253 Mama anayeketi moja kwa moja nyuma yetu pale, yuna uvimbe wa neva. Unaamini kwamba Mungu ataponya uvimbe wako wa neva, mama?

254 Huyu hapa mama mmoja aliyevaa koti dogo, koti jekundu, hapa. Ameketi pale. Ana ugonjwa wa mapindi, pia. Unaamini kwamba Mungu atauponya ugonjwa wako wa mapindi? Inua mkono wako, kama unaamini.

255 Mtu yeyote humu ndani anayeamini ya kwamba tabia za Yesu Kristo zimo miongoni mwetu, usiku wa leo, inua mkono wako, useme, "Ninaamini hilo." [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Ninaamini hilo!"—Mh.]

256 Wote walio humu ndani, mtakaomkubali Yeye kama mponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu, na kusema, "Ninaamini hilo." Amkeni. Simameni, kutoka vitini mwenu, chochote kile. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawapeni Yeye, katika Jina la Bwana Mungu.

Mungu Akijitambulisha Mwenyewe Kwa Tabia Zake SWA64-0320
(God Identifying Himself By His Characteristics)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 20 Machi, 1964, katika Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Denham Springs huko Denham Springs, Louisiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org